

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini

## TAARIFA KWA UMMA TAHADHARI DHIDI YA UDANGANYIFU

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawakumbusha watoa huduma za usafiri kuchukua tahadhari dhidi ya matapeli wanaojitambulisha kuwa ni wafanyakazi wa LATRA. Matapeli hao huwalaghai waombaji leseni za usafirishaji kuwa ni vigumu kupata leseni za usafirishaji.

2. Watoa huduma za usafirishaji mnakumbushwa kuendelea kutuma maombi ya leseni kwa kutumia mfumo wa RRIMS kwa anwani ya **[rrims.latra.go.tz](http://rrims.latra.go.tz)**

3. Mamlaka inatoa wito kwa watoa huduma za usafiri na wadau wote kufichua vitendo vya utapeli/udanganyifu kwa kupiga simu nambari 0800110019/20 au kwa ujumbe mfupi wa maandishi au WhatsApp kupitia namba: +255 734 220 000.

Pia waweza kutoa taarifa kwa barua kupitia anwani: Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, S.L.P 3093, Dar es Salaam. Barua pepe: [malalamiko@latra.go.tz](mailto:malalamiko@latra.go.tz)

4. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo vya udanganyifu.

Imetolewa na;

Mkurugenzi Mkuu,

**Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini**

25 Februari, 2022